



**KANUNI YA MAADILI YA MWOMBAJI**

**MAELEZO KUHUSU MAHOJIANO YAKO YA MTANDAONI YA ULINZI WA  
KIMATAIFA**

Umeomba ulinzi wa kimataifa katika Jimbo hili na umeipatia Ofisi hii taarifa zinazohusu dai lako katika fomu yako ya maswali. Lengo la mahojiano ya mtandaoni ya ulinzi wa kimataifa ni kuchunguza maelezo kamili ya dai lako kutoka maelezo ambayo tayari yametolewa na maelezo ambayo utatoa wakati wa mahojiano yako ya mtandaoni. Hili litahitaji maswali ya kina kuhusu masuala ambayo uliyaaisha katika fomu yako ya maswali na maswala mengine yoyote ambayo mhojaji anadhani ni muhimu. Unapaswa kutafuta ufafanuzi kutoka kwa mhojaji kuhusu maswali yoyote uliyoyaulizwa ambayo huelewi.

Unapaswa kueleza kwa uwazi na kwa kina hofu zako na kutoa maelezo yote na taarifa zote ambazo ni muhimu kuhusu hali yako mahususi. Mahojiano ni fursa yako ya kueleza kwa undani ni kwa nini unahofia kurudi katika nchi yako ya asili.

Ni **wajibu wako kushirikiana kikamilifu na kuwa mkweli kabisa**. Rekodi iliyoandikwa ya mahojiano ya mtandaoni itahifadhiwa na mhojaji ya vipengele muhimu na vinavyoweza kuwa muhimu vya dai lako. Rekodi ya mahojiano itasomwa kwako na kupigwa muhuri wa wakati katika wakati wa mahojiano ya mtandaoni na hii ni fursa kwako ya kusahihisha maelezo yoyote ambayo unadhani hayakurekodiwa kwa usahihi. Utaulizwa kuthibitisha kwa mdomo kwamba unakubaliana na rekodi ya makubaliano wakati wa mahojiano yako na hii itapigwa muhuri wa wakati kwenye rekodi. Muhuri wa wakati unaonyesha uthibitisho wa mdomo na wakati/tarehe yake.

Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa, kwa hali yoyote iwezekanayo, haitawasiliana na viongozi wa nchi ambayo unaikimbia.

Kufuatia mahojiano, pendekezo litatolewa kuhusiana na ombi lako na ikiwa hilo pendekezo litakuwa hasi, utakuwa na fursa ya kukata rufaa kwa Mahakama ya Rufaa ya Ulinzi wa Kimataifa.

**Wajibu wa Mkalimani:** Mkalimani, akiwepo, atatafsiri maswali ya mhojaji na majibu yako kwa usahihi. Mkalimani hatatoa ushauri kwako na wala hatatoa maoni yoyote kuhusu ubora wa kesi yako. Mkalimani anafahamu hali ya usiri wa mahojiano. Mkalimani haruhusiwi kuingia katika mazungumzo pamoja na wewe isipokuwa tu kupitia mhojaji.

**Mwakilishi wa Kisheria:** Mwakilishi wako wa kisheria, akiwepo, anaweza kuchukua vidokezo lakini hapaswi kukatisha au kujibu maswali yoyote kwa niaba yako. Mwishoni mwa mahojiano, mwakilishi wako wa kisheria ataombwa ikiwa ana maoni yoyote ya kutoa.

Utaombwa kuthibitisha kwamba umesoma na kuelewa hati hii mwanzoni mwa mahojiano yako.

**Jina la mwombaji:**

**Tarehe iliyokubaliwa: TAREHE/MWEZI/MWEZI**

**Wakati uliokubaliwa: TAREHE/MWEZI/MWAKA**